**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

*Simu Na-+255262963470*
*Fax:+255262963117*
*E-mail:ps@mit.go.tz*
*Website-www.mit.go.tz*

Mji wa Serikali,
Mtaa wa
Viwanda,
S.L.P 2996,
**DODOMA**

## TAARIFA KWA UMMA

## TAARIFA YA NIA YA SERIKALI KUTANGAZA MAZAO YANAYOTUMIA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA KWENYE GAZETI LA SERIKALI

Mfumo wa Stakabadhi za Ghala umepata mafanikio makubwa tangu Sheria ya Stakabadhi za Ghala Namba 10 ya Mwaka 2005 ilipoanza kutumika, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuwezesha wakulima kupata bei za ushindani sokoni, kuongeza usimamizi wa ubora wa mazao, matumizi ya vipimo rasmi, kujenga mifumo imara ya kitaasisi ya kusimamia masoko ya mazao hususan Vyama vya Ushirika, kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno na kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Aidha, Serikali inaendelea kuimarisha utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa mazao na bidhaa zingine zaidi. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara ya Viwanda na Biashara inatarajia kuandaa **Tangazo la Serikali** kwa mujibu wa Kifungu cha 2 cha Sheria ya Stakabadhi za Ghala Na 10 ya 2005 na marekebisho yake ambacho kinamruhusu Waziri mwenye dhamana na biashara kutangaza kwenye ***Gazeti la Serikali*** mazao yatakayotumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Kabla ya Wizara kutoa tangazo la Serikali inapenda kupokea maoni ya wadau kuhusu mazao yanayopendekezwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Orodha ya mazao yanayopendekezwa ni kama ifuatavyo:

- ***i.*** ***Kahawa (Coffee),***
- ***ii.*** ***Chai kavu (Tea),***
- ***iii.*** ***Pamba (Cotton),***

*iv. Mkonge (Sisal),*
*v. Korosho ghafi, (Raw Cashewnut)*
*vi. Ufuta (Sesame/sim sim),*
*vii. Mahindi (White maize),*
*viii. Mpunga (Paddy),*
*ix. Ngano (Wheat),*
*x. Shayiri (Burley),*
*xi. Mtama mweupe (Sorghum),*
*xii. Alizeti (Sunflower),*
*xiii. Kakao (Cocoa),*
*xiv. Maharage ya soya (Soya beans),*
*xv. Mbaazi (Pegion peas),*
*xvi. Choroko (Green gram),*
*xvii. Dengu (Chick peas),*
*xviii. Karanga (Groundnuts),*
*xix. Vitunguu swaumu (Garlic),na*
*xx. Ngozi (Hides & skin),*

Kutokana na tahadhari ya uwepo wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu (COVID-19), Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala itakusanya maoni ya wadau kwa njia ya kielektroniki kupitia barua pepe info@wrrb.go.tz, au whatsapp namba 0715 568 444 kuanzia tarehe ya tangazo hili. Tafadhali unaombwa kuwasilisha maoni yako kabla ya tarehe 30 Juni, 2020.

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na Bw. Fidelis Temu kwa namba ya simu **0715 568 444.**

Imetolewa na
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
**Wizara ya Viwanda na Biashara**
13 Mei, 2020